

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: +255 26 2322129
Nukushi: 255 26 2322128
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba, Dodoma,
2 Mtaa wa Michezo,
S. L. P 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

KUPANGIWA MAJUKUMU MENGINE MENEJA WA UWANJA WA MKAPA

Agosti 09, 2022 – Dodoma

Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa leo, Agosti 9, 2022 amemuagiza Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni Sanaa na Michezo. Dkt, Hassan Abbasi kumpangia majukumu mengine Meneja wa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Bw. Godon Nsajigwa.

Taarifa iliyotolewa na Dkt. Abbasi inasema kuwa Meneja huyo anapangiwa majukumu mengine kwa kushindwa kusimamia matumizi endelevu ya Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Akieleza utekelezaji wa agizo hilo, amesema tayari taratibu zimekwishaanza za kupangiwa majukumu mengine na nafasi hiyo inatarajiwa kujazwa mara moja.

A handwritten signature in blue ink, appearing to read 'John Mapepe'.

John Mapepele

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

